

MKOA WA DAR ES SALAAM

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UCHAGUZI WA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2018 KATIKA MKOA WA DAR ES SALAAM

Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na jumla ya wanafunzi **66,978** waliosajiliwa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka huu 2017. Kati yao wavulana ni **31,911** na wasichana **35067**. Idadi ya watahiniwa waliofanya mtihani huo ni **66,695** sawa na asilimia **99.58**, kati yao wavulana ni **31,760** na wasichana ni **34,935**. Watahiniwa **283** sawa na asilimia **0.42** hawakufanya mtihani huo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo utoro wanafunzi **241**, vifo **15**, ugonjwa **17** na sababu zingine **10**. Idadi ya wasiofanya imeshuka kutoka wanafunzi **715** mwaka 2016 hadi wanafunzi **283** mwaka 2017.

Watahiniwa **58,573** (Wavulana **28,103** na wasichana **30,470**) sawa na asilimia **87.82** wamefaulu mtihani huo. Ufaulu huo umepanda kutoka asilimia **82.58** ya mwaka 2016 hadi asilimia **87.82** kwa mwaka 2017 sawa na asilimia **5.24**. Matokeo hayo yameufanya Mkoa wa Dar es Salaam kuwa katika nafasi ya kwanza (**01**) Kitaifa. Aidha, wanafunzi wote **58,573** waliofaulu sawa na **100%** wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza Januari, 2018 hivyo kwa mwaka huu hatutakuwa na chaguo la pili.

